JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA ZA WATENDAJI WA VITUO VYA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATA YA NYARERO WA MWAKA 2026

Kwa madhumuni ya uendeshaji wa uchaguzi Mdogo na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, kikisomwa pamoja na kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Mkurugenzi wa Uchaguzi anakaribisha maombi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo; -

1. **Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura.**
2. **Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kupigia Kura.**
3. **Makarani Waongozaji Wapiga Kura.**

A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI ZA WASIMAMIZI AU WASIMAMIZI WASAIDIZI WA VITUO VYA KUPIGIA KURA

(a) awe raia wa Tanzania;

(b) ametimiza umri wa miaka 18 au zaidi;

(c) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa;

(d) awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

(e) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kingereza. Pia, anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na

(f) ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kusimamia upigaji kura na kuhesabu kura.

B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA

(a) awe raia wa Tanzania;

(b) Ametimiza umri wa miaka 18 au zaidi;

(c) awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;

(d) ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanyia kazi;

(e) awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

(f) awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuandika na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura na Walinzi wa Vituo;

(g) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na

(h) awe na uelewa wa matumizi mazuri ya lugha katika kutoa huduma kwa mteja (mpiga kura).

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -

i. Siku ya Uchaguzi Msimamizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi **70,000/=** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi **20,000/=** kwa siku moja na nauli Shilingi **20,000/=**.

ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi **65,000/=** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi **20,000/=** kwa siku moja na nauli Shilingi **20,000/=**.

iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Shilingi **65,000/=** kwa siku mbili, posho ya chakula Shilingi **20,000/=** kwa siku moja na nauli Shilingi **20,000/=**.

iv. Wakati wa mafunzo watendaji wote watalipwa posho ya kiasi cha Shilingi **50,000/=** kwa siku na nauli kiasi cha Shillingi **20,000/=** kwa kila siku ya mafunzo. Mafunzo kwa wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo yatafanyika kwa muda wa siku mbili, na mafunzo kwa makarani waongozaji wapiga kura yatafanyika kwa muda wa siku moja.

D. MASHARTI YA JUMLA

i. Mwombaji lazima aainishe nafasi anayoomba pamoja na kata anayoomba kufanyia kazi; na

ii. Mwombaji awe tayari kufanya kazi katika kituo chochote atakachopangiwa.

iii. Mwombaji aambatishe: -

a. nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na Taaluma ikiwa anavyo.

b. wasifu (CV) ukionesha anuani yake ya makazi, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini wake wawili na namba zao za NIDA.

c. picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyomo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.

d. barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa serikali ya mtaa au kijiji katika eneo analoishi.

iv. Mwombaji ambaye ni mtumishi wa umma apitishe barua yake ya maombi kwa mwajiri wake.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo: -

Msimamizi wa Uchaguzi

Jimbo la Tarime Vijijini,

S.L.P 16,

TARIME.

KUWASILISHA MAOMBI NI TAREHE 14 HADI 20 OKTOBA, 2026.

Limetolewa leo tarehe 14 Oktoba, 2026 na : -

.....

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

ME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA TARIME
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME